336/2
KSWAHILI
KARATASI YA PILI
Saa mbili

# WUNNA EDUCATIONAL SERVICES

# LEARNERS' ASSESSMENT BOARD (WESLAB)

*Uganda certificate of Lower secondary education*

MITIHANI YA MWISHO WA MUHULA WA KWANZA
Kidato cha tatu
KISWAHILI
Karatasi ya Pili
Ufahamu na Uchambuzi wa Fasihi

MUDA: SAA MBILI

**MAAGIZO;**

- ✓ *Karatasi hii ina sehemu mbili; A na* ***B***
- ✓ *Maswali yote* ***mawili*** *ni ya* ***lazima***
- ✓ *Majibu yote yaandikwe kwenye karatasi uliyopewa*

©WESLAB 2025
**Download research notes & assessments from our website**
wunnaeducationalservices.com

**SEHEMU A**
**UFAHAMU**

1. Soma taarfa hii kisha ujibu maswali yanayofuatia. *(uzito **20)***

*Takribani* watu milioni tatu duniani hufa kila mwaka kwa sababu ya magonjwa yanayotokana na tumbaku. Mojawapo ya magonjwa hayo ni saratani au kansa ya mapafu. *Yamkini* kila mwaka watu wengi hupatwa na saratani hiyo.

Kama yalivyo magonjwa mengine, saratani huwapata wanaume na wanawake. Hata hivyo, wanaume hupatwa sana na saratani ya mapafu,tumbo na machango, zaidi na saratani ya matiti au maziwa, uzazi,tumbo na mapafu.

Wataalamu wa kansa hudai kwamba kati ya aina hizi zote zilizotajwa hapo juu, saratani ya mapafu ndiyo inayopatikana kwa wingi zaidi miongoni mwa wanawake na wanaume ikifuatwa na saratani ya tumbo.

Je,saratani ya mapafu husababishwa na nini hasa? Wataalamu wa magonjwa ya kansa wanadai kwamba kuna uhusiano dhahiri kati ya kansa ya mapafu na uvutaji wa sigara. Yaani kuvuta sigara au kiko kunaweza kusababisha saratani. Tafiti nyingi zilizofanywa zimethibitisha bila tashwishi yoyote kwamba kuna uhusianao kati ya uvutaji sigara na kansa ya mapafu.

Ingawa uhusiano wa tumbaku na kansa ni jambo linalojulikana, ni jambo la kustaajabisha kwamba mpaka leo watu wengi wanaendelea kuvuta sigara.

Kama tunavyojua, tumbaku inaweza kutumiwa kwa njia tofautitofauti.Kwa mfano, kuna uvutaji wa sigara, sigara kubwa au sigaa,viko na kadhalika. Pia kuna utafunaji na unusaji wa tumbaku. Ingawa kuna njia zote hizi za utumiaji wa tumbaku, utafiti mwingi uliofanywa kuhusu kansa unahusu uvutaji na sio matumizi yale mengine ya tumbaku.

Je, kansa imeenea kiasi gani?

tu. Wakati huo kulikuwa na wengi wenye kansa ya mapafu. Miongoni mwa. wanawake wengi walivyoendelea kuvuta sigara ndivyo visa vya kansa vilivyoongezeka miongoni mwao.

Katika nchi zilizoendelea, ambako watu wanavuta sigara kwa wingi, elimu inayohusu madhara ya uvutaji sigara imeshika kasi. Kutokana na elimu hivyo, jambo linalosikitisha ni kwamba, huku uvunataji wa sigara unapoonyesha dalili za kupungua katika nchi zilizoendelea,uvutaji sigara *umepamba moto* katika nchi zinazoendelea kushinda nchi zilizoendelea.

Tunapozungumzia uvutaji sigara aghalabu huwa tunamfikiria yule mwenye kuivuta lakini hatufikirii wale wanaoshirikishwa kweny uvutaji pili kupenda kwao. Hebu tumfikirie mke alyeolewa na mvutaji sigara,tuwafikirie pia watoto wa mtu huyo na wageni wake pia. Wafikirie wateja wanaopuliziwa moshi hotelini. Hawa wote wanashirikishwa katika uvutaji wa sigara bila hiari yao.

©WESLAB 2025
**Download research notes & assessments from our website**
wunnaeducationalservices.com

Kwa sababu ya madhara yanayotokana na uvutaji wa sigara, hatua fulani huchukuliwa na serikali mbalimbali kupunguza uvutaji na kuwalinda watu wasiovuta sigara kutokana na wavutaji wasiojali. Pakiti za sigara kwa mfano, huwa na onyo kutoka kwa wizara ya afya kwamba:*sigara ni hatari kwa maisha ya mwanadamu.* Serikali nyinginezo zimepiga marufuku uvutaji wa sigsra hadharani kama kwenye mabasi ya kusafiria,gari moshi,n ahata kwenye mahoteli. Ili kulinda watu wasiovuta sigara kweye ndege,gari la moshi na kwingineko, kuna mahali palipotengewa wavutaji sigara.

Maswali

a) Ipe taarifa hiyo anwani mwafaka.

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

b) Je,ni aina ipi ya saratani inayopatikana zaidi miongoni mwa wanawake na wanaume?

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

c) Kati ya njia za utumiaji wa tumbaku zinazojulikana, ni ipi iliyokwisha fanyiwa utafiti kwa mujibu wa taarifa?

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

d) Mbona visa vya kansa havikuwa vingi miongoni mwa wanawake hapo zamani?

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

e) Mtu anawezaje kushirikishwa katika uvutaji wa sigara pasipo kupenda kwake?

©WESLAB 2025

**Download research notes & assessments from our website**

wunnaeducationalservices.com

..............................................................................
..............................................................................
..............................................................................
..............................................................................
..............................................................................

f) Je,mwandishi anamaanisha nini kwa kutumia maneno yafuatayo?

i) Takribani

..............................................................................
..............................................................................
..............................................................................

ii)Nadra

..............................................................................
..............................................................................
..............................................................................
..............................................................................

iii)Uvutaji wa sigara umepamba moto

..............................................................................
..............................................................................
..............................................................................

**SEHEMU B**

**UCHAMBUZI WA FASIHI**

2. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yatakayofuata. *(uzito 20)*

Jameni sikilizeni,shairi nishalitunga,
Sikio nakuombeni, nipatie bila pinga,
Ni ukweli si utani, kwa mkubwa na mchanga,
Ulema si upungufu, hakika pata kujua.

Aliye nao ulema, karibu fika jamani,
Usijione yatima, u muhimu kama ini,
Mungu hapa kakutuma, kukujazia maoni,
Ulema si upungufu, hakika pata kujua.

Kilema aweza jenga, jamii nzuri jamani,
Mambo muhimu apanga, akishapewa amani,
Hebu apewe utamu, na maisha ya thamani,
Ulema si upungufu, hakika pata kujua.

©WESLAB 2025
**Download research notes & assessments from our website**
wunnaeducationalservices.com

Azifanya zote kazi, upungufu mi sioni,
Ni kweli na sichezi, la maana si utani,
Hebu apewe utamu,na maisha ya thamani,
Ulema si upungufu, hakika pata kujua.

**Maswali**

a) Chambua muundo wa nje wa shairi hilo.

……………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………

b) Fafanua angalau mafunzo matatu unayopata katika shairi hilo.

……………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………

c) Elezea hisia unayopata baada ya kusoma shairi hilo.

……………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………

d) Toa maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katiaka shairi hilo.

i) Utani

……………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………

ii) Thamani

……………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………

iii)Duni

……………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………

mwisho

Nyuma haturudi

©WESLAB 2025
**Download research notes & assessments from our website**
wunnaeducationalservices.com